

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Barua pepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Dar es Salaam
11 Agosti, 2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amewapangia vituo vya kazi Mabalozzi wakiwemo Mabalozzi Wateule (06) aliowateua tarehe 10 Mei, 2023. Aidha, Mhe. Rais amewabadilisha vituo vya kazi Mabalozzi wanne (04). Mabadiliko hayo ni kama ifuatavyo:

A. Mabalozzi waliopangiwa vituo vya kazi:

- i) Balozi Fatma Mohammed Rajab kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Oman. Balozi Rajab anachukua nafasi ya Balozi Abdallah Abasi Kilima ambaye amestaafu.
- ii) Balozi Joseph Edward Sokoine kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Canada. Balozi Sokoine anachukua nafasi ya Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya ambaye mstaafu.
- iii) Balozi Naimi Sweetie Hamza Aziz kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Austria.
- iv) Meja Jenerali Ramson Godwin Mwaisaka (Balozi Mteule) kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Rwanda. Meja Jenerali Mwaisaka anachukua nafasi ya Balozi Meja Jenerali Richard Mutayoba Makanzo ambaye amehamishiwa Cairo, Misri.
- v) Bw. Gelasius Gaspar Byakanwa (Balozi Mteule) kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Burundi. Bw. Byakanwa anachukua nafasi ya Balozi Jilly Maleko ambaye amestaafu.
- vi) Bw. Habibu Awesi Mohamed (Balozi Mteule) kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Qatar. Bw. Mohamed anachukua nafasi ya Balozi Mahadhi Juma Maalim ambaye amehamishiwa Kuala Lumpur, Malaysia.
- vii) Bw. Imani Salum Njalikai (Balozi Mteule) Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Algeria. Bw. Njalikai anachukua nafasi ya Balozi Meja Jenerali Jacob Gideon Kingu ambaye amestaafu.

- viii) Bw. Hassan Iddi Mwamweta (Balozi Mteule) Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ujerumani. Bw. Mwamweta anachukua nafasi ya Balozi Abdallah Saleh Possi ambaye amehamishiwa Geneva, Uswisi.
- ix) Dkt. Mohamed Juma Abdallah (Balozi Mteule) kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Saudi Arabia. Bw. Abdallah anachukua nafasi ya Balozi Ali Jabir Mwadini ambaye amehamishiwa Paris, Ufaransa.

B. Mabalozzi waliohamishwa vituo

- i) Balozi Ali Jabir Mwadini kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Ufaransa. Balozi Mwadini anachukua nafasi ya Balozi Dkt. William Shelukindo ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.
- ii) Balozi Meja Jenerali Richard Mutayoba Makanzo kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Misri. Balozi Meja Jenerali Makanzo anachukua nafasi ya Balozi John Emmanuel Nchimbi ambaye anarejea nyumbani.
- iii) Balozi Abdallah Saleh Possi kuwa Mwakilishi wa Kudumu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ofisi za Umoja wa Mataifa Geneva, Uswisi. Balozi Possi anachukua nafasi ya Balozi Maimuna Tarishi ambaye amemaliza mkataba wake.
- iv) Balozi Dkt. John Stephen Simbachawene kuwa Balozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Uganda. Balozi Simbachawene anachukua nafasi ya Balozi Dkt. Aziz P. Mlima ambaye amestaafu.

Mabalozzi Wateule wataapishwa tarehe 16 Agosti, 2023 saa 05:00 asubuhi Ikulu, Chamwino - Dodoma.



Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu